



Cour
Pénale
Internationale

International
Criminal
Court

ICC-PIDS-FS-06-008/10_Swa

Ofisi ya Prezidenti na Vyumba



Biro ya Prezida ya Mahakama ya Kimataifa
ya Jinai
Foto: ICC- CPI/Max Koot

Biro ya Prezida na Machumba

Biro ya Prezida, ni moya kati ya bipande ine bya Mahakama. Hii masiku inaundwa na Prezida Sang-Hyun Song (Jamhuri ya Korea), makamu wa kwanza wa prezida Fatoumata Dembele Diarra (Mali) na makamu wa pili wa prezida Hans-Peter Kaul (Ujerumani). Balichaguliwa, siku 11 mwezi ya tatu 2009, kwa kura ya wingi ulio dhahiri ya bajije ba Mahakama juu ya batumike ku Biro ya Prezida muda ya miaka tatu.

Biro ya Prezida iko na kazi ya kuongoza muzuri Mahakama yote, kuacha tu Biro ya Prokirere. Lakini inatumikaka pamoja na Biro ya Prokirere na inaiombaka shauri ku byenye binaangalia mafaa ya bote. Madaraka ya uongozi ya Biro ya Prezida ni sawa vile kusimamia kazi ya Biro ya Grefye tena kufanya kwa ginsi Biro ya Grefye itumikie muzuri Machumba. Kati ya kazi zake za kusimamia, Biro ya Prezida inasaidia ku maneno mingi ya uongozi na inapana njia ya kufuata mu maneno yenye kuangalia uongozi ya Mahakama kwa jumla, sawa vile Kanuni za utumishi, siri ya habari na Mfuko wa Dhamana wa Mahakama.

Mu kazi za Biro ya Prezida muko vile vile kazi za kimahakama na uhusiano na inje. Mukufanya kazi zake za kimahakama, Biro ya Prezida inapangaka kazi ya kimahakama za Machumba na kufanya mapashwa yenye Mkataba wa Roma, Kanuni za Utaratibu na Ushahidi na tena Kanuni za Mahakama zinaomba.

Ndani ya kazi za Biro ya Prezida za uhusiano na inje kuko kutafuta na kufanya makubaliano ku jina ya Mahakama na kufanya kwa ginsi batu bajuwe Mahakama.

Machumba

Sawa vile artikle 39-1 ya Makataba wa Roma inasema, Machumba ziko ndani ya matawi. Zinashurulika na kazi za kimahakama za Mahakama. Kuko matawi tatu : Tawi la utangulizi, Tawi la kesi na Tawi la rufaa.

Kusema tawi jije atatumika ndani inafuata na kazi kila jije atatumika na ujuzi na uzoefu ya jije. Hii inafanyika kwa ginsi kila tawi ikuwe na bataalamu ba sheria yenye kuangaliana na maenfraksyo na sheria ya ginsi ya kuongoza masambo yenye kuangaliana na maenfraksyo na sheria ya kimataifa. Bajije benye banatumika ku Tawi la rufaa banafanya kazi mu ile Tawi tu muda yote ya kazi yabo.

Biro ya Prezida inaweza kuamua kuunda machumba zingine za utangulizi wala machumba zingine za kesi, kama uzito ya kazi ya Mahakama inaomba vile, na juu ya uongozi muzuri. Inaweza vile vile kusema jije wa mu Tawi la kesi atumike kwa muda mu Tawi la utangulizi wala wa mu Tawi la utangulizi atumike kwa muda mu Tawi la kesi. Kila tawi inachaguuka prezida wake, yeye njo anaongozaka tawi muda wa mwaka moya.

Tawi la utangulizi

The Pre-Trial Division is composed of judges with Tawi la utangulizi linaundwa na bajije benye banazoweya sana masambo yenye kuangaliana na maenfraksyo. Bajije banatumika muda ya miaka tatu. Hii masiku kuko machumba mbili za utangulizi.

Kila chumba ya utangulizi kiko na bajije tatu, ata kama jije moya anaweza kufanya kazi fulani fulani za ile chumba. Jije prezida wa chumba anachaguliwa na bajije ba mu ile chumba.

Moya kati ya kazi za Chumba cha utangulizi ni kupatia Biro ya Prokirere ruhusa ya kuanza ankete ao kukatala kuipatia ruhusa ya kufanya vile. Inaangaliaka kwanza kama afere iko ndani ya uwezo wa kisheria wa Mahakama, bila kuzuia hatua zenye Mahakama itakamata nyuma juu ya uwezo wa kisheria na kukubalika.

Kufuatana na Mkataba wa Roma, kama “faida ya sheria” njo msingi ya uamuzi ya Prokirere, Chumba cha utangulizi kinaweza ku nia yake pekee, wala kufuatana na ombi ya inchi yenye ilituma hali kwa Prokirere wala ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kuangalia ile uamuzi ya Prokirere ya kukatala kuanza ankete wala kushtaki.

Ni kazi ya Chumba cha utangulizi kufanya, kutokana na ombi ya Prokirere, manda ya kukamata wala samansi ya kuita mutu kufika mbele ya Mahakama na kuheshimisha haki za batu bote mu kipindi ya ankete. Chumba kinakamataka vile vile mipango juu ya kuchunga haki ya batu bengine benye bako mu masambo na, kama ni lazima, kuchunga usalama na heshima ya maisha ya pekee ya baviktime na ba temwe. Kinachungaka ushahidi, bafungwa wala batu benye balifika mbele ya Mahakama kufuatana na samansi, na habari zenye kuangaliana na usalama ya inchi.

Ndani ya muda ya kufaa, kisha mwenye banawazia iko na kosa kutolewa ku Mahakama, wala kufika mbele ya Mahakama ku utashi yake, Chumba cha utangulizi inafanyika mkusanyo ya masambo kwenye Prokirere na mtu mwenye banawazia kama alifanya kosa na/wala avoka wake batakuwa, juu ya kuhakikisha mashtaka wala apana. Mkusanyo ya masambo ya kuhakikisha mashtaka inaweza kufanyika bila mtu mwenye banawazia alifanya kosa kukuwa pale.

Tawi la kesi

Bengi kati ya bajije ya Tawi la kesi banazoweya sana masambo yenye kuangaliana na maenfraksyo. Banatumika ndani ya hii Tawi muda ya miaka tatu wala mpaka kumaliza afere kama masambo ilishaanza. Hii masiku kuko machumba mbili za kesi.

Kama mashtaka inahakikishwa na Chumba cha utangulizi, Biro ya Prezida inaunda Chumba cha kesi juu ya kufuatilia ile afere.

Kila chumba cha kesi iko na bajije tatu, jije prezida wa chumba anachaguliwaka na bajije ba mu ile chumba. Jije moya anaweza kufanya kazi fulani fulani za ile chumba.

Kazi ya kwanza ya Chumba cha kesi ni kufanya kwa ginsi masambo ikuwe ya haki na ya haraka, na mu heshima kabisa ya haki ya mwenye kushtakiwa na ya usalama ya baviktime na batemwe.

Masambo inafanyikaka mbele ya batu bote, na mwenye kushtakiwa anakuwaka pale. Lakini mu hali ya pekee kunaweza kuwa masambo bila batu ya inje kuona wala kusikia juu ya kuinga habari za siri wala nyeti zenye ziko mu maneno yenye ilielezwa wala juu ya kuchunga

baviktime na batemwe. Jijema inasomewaka wakati ya mkusanyo ya masambo mbele ya batu bote.

Chumba cha kesi kinaamuaka kama mwenye kushtakiwa iko na kosa wala apana, na kinaweza kama ule mutu anapatikana na kosa, kumupa malipizi ya kufungwa muda yenye haiwezi kupita miaka makumi tatu, wala kama kuko uzito kabisa, malipizi ya kufungwa maisha yote. Malipizi ya kulipa makuta nayo inaweza kutolewa. Chumba cha kesi kinaweza kusema baviktime bapate malipo sawa vile, kubarudishia bitu yabo, kubalipa makuta na kubarudishia heshima.

Sawa vile imesemwa hapa yulu, Biro ya Prezida inaweza kusema jije wa Tawi la utangulizi atumike kwa muda mu Tawi la kesi kama kazi ya Mahakama inaomba kufanya vile, lakini jije mwenye alikuwa mu hatua za mwanzo za afere hawezi kusambisha mu chumba cha kesi yenye iko inafuatilia ile afere.

Tawi la rufaa

Chumba cha rufaa inaundwa na bajije tano ba mu Tawi la rufaa, abo njo banachaguaka jije prezida ku kila apele.

Hii Tawi inashurulikaka na apele kutoka kwa mtu mwenye amehukumiwa, kwa Prokirere, ku benye kusimamia ba viktime mbele ya sheria wala kwa mtu wa roho mzuri mwenye kitu kimeguswa na uamuzi ya Mahakama.

Mtu mwenye amehukumiwa anaweza kufanya apele ya kupinga kupatikana kwake na kosa na ya kupinga malipizi. Prokirere anaweza kufanya apele ya uamuzi ya kusema mtu hana kosa wala ya kuhukumu mwenye kushtakiwa, wala kufanya apele ya kupinga malipizi. Ile apele inaweza kufanyika kutokana na kosa la kiutaratibu, kosa la ukweli wala kosa la kisheria, wala kutokana na sababu ingine yoyote yenye kuangaliana na usawa na kuaminika ya masambo wala ya uamuzi. Chumba cha rufaa kinaweza kuvunja wala kubadilisha uamuzi ya kuhukumu wala malipizi na kuamuru kukuwe masambo ya mupya mbele ya Chumba kingine cha kesi. Kinaweza vile vile kubadilisha uamuzi ya mwisho ya kuhukumu wala malipizi.

Chumba cha rufaa kinaangaliaka upya malipizi. Kwa mfano, wakati mtu mwenye amehukumiwa anaisha kupitisha mbili juu ya tatu ya malipizi yake wala kufanya miaka 25 mu prizo kama alihukumiwa kufungwa maisha yote, Chumba kitasema kama inawezekana kupunguza malipizi yake. Kikasema kama haiwezekane kupunguza malipizi, Chumba cha rufaa kitaangalia tena, kila miaka tatu, kama inawekana wala apana. Tena, Chumba cha rufaa njo kiko na uwezo ya kuamua juu ya kukataliwa kwa Prokirere wala makamu wa prokirere.

Benye kusimamia baviktime mbele ya sheria, mtu mwenye amehukumiwa wala mtu wa roho mzuri mwenye kitu kimeguswa na uamuzi banaweza kufanya apele juu ya uamuzi ya malipo ku baviktime. Apele inaweza vile vile kuwa juu ya kupinga uamuzi ingine ya Chumba cha utangulizi yenye kufanyika wakati ya kuendesha masambo, inaweza kuangaliana na uwezo wa kisheria na kukubalika.